**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA**

**MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI**

**711** **KISWAHILI**

**Muda: Masaa 3** **Ijumaa, 05th May 2006 Asubuhi**

---

**Instructions.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali kumi na sit (16).

2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na maswali mawili kutoka kila sehem **B** na **C**.

3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** Zina jumla ya alama **sitini (60).**

4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha majibu.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii. Kila swali kina alama nne (4).

1. (a) Eleza maana ya silabi na toa aina mbili za silabi kwa mfano mmoja mmoja.
   (b) Andika maneno manne ambayo yana silabi mbili.

2. Fafanua maana ya sarufi ya Kiswahili na eleza dhima zake tatu katika matumizi ya lugha.

3. Eleza maana ya kitenzi kikuu na taja vitenzi viwili vya mfano katika sentensi sahihi.

4. Kwa kutumia sentensi, onesha matumizi ya kiambishi cha nafsi ya kwanza umoja, nafsi ya pili wingi, nafsi ya tatu umoja na nafsi ya tatu wingi.

5. Eleza aina nne za maneno kwa kuzingatia kazi yake katika sentensi na toa mfano mmoja mmoja kwa kila aina.

6. (a) Eleza maana ya sentensi sahili.
   (b) Tunga sentensi sahili nne zenye kauli tofauti.

7. Taja sifa nne za lugha ya Kiswahili kama lugha ya kitaifa kwa kuzingatia hali ya kijamii nchini Tanzania.

8. Toa maana ya istilahi zifuatazo kwa muktadha wa fasihi:
   (a) Mandhari
   (b) Wahusika
   (c) Mtindo
   (d) Dhamira

9. Eleza kwa mifano namna Kiswahili hutumika katika:
   (a) Biashara
   (b) Elimu
   (c) Teknolojia
   (d) Afya

10. Fafanua maana ya mofimu tegemezi na eleza kwa kutumia mifano miwili jinsi inavyoathiri uundaji wa maneno.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama 15.

11. Eleza hatua sita anazopaswa kufuata mwalimu katika kufundisha somo la Kiswahili kwa kutumia mbinu ya kazi za vikundi.

12. Jadili kwa hoja tano namna ushairi wa Kiswahili unavyoweza kutumiwa kufundisha maadili kwa wanafunzi wa sekondari.

13. Kwa hoja tano, eleza umuhimu wa kufundisha uandishi wa barua za kirafiki kwa wanafunzi wa sekondari.

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama 15.

14. Tathmini athari chanya tatu na hasi tatu za matumizi ya Kiswahili katika vyombo vya habari nchini Tanzania.

15. Eleza kwa hoja sita jinsi lugha ya Kiswahili inavyoweza kutumika kama chombo cha maendeleo ya kiuchumi katika jamii ya Watanzania.

16. Linganisha kazi ya riwaya na tamthilia kama kazi za fasihi kwa kutumia hoja sita zinazojikita katika muundo, lugha na uwasilishaji wa maudhui.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org